

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI



MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)



TAARIFA KWA UMMA

KUCHUKUA BIDHAA ZA MAFUTA KUTOKA BANDARI YA TANGA

Serikali ilianzisha matumizi ya Bandari ya Tanga ikiwa ni eneo la miundombinu la pili ya kupokelea bidha za mafuta baada ya Bandari ya Dar es Salaam. Pia Serikali ilianzisha matumizi ya Bandari ya Mtwara kama eneo la miundombinu ya tatu kwa ajili ya kupokea mafuta ili pamoja na mambo mengine, kupunguza gharama za kufanya biashara nchini. Kutokana na hatua hii, Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) na wadau wa biashara ya mafuta wamekuwa wakitumia bandari hizo tatu.

Hata hivyo, pamoja na juhudi nzuri za Serikali, EWURA imegundua kuwepo kwa baadhi ya wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara walioanza kununua mafuta kutoka Bandari ya Dar es Salaam na kuyasafirisha kwa ajili ya matumizi katika mikoa hiyo. Hatua hii ova imewaathiri wauzaji mafuta ya jumla wanaoingiza kupitia Bandari ya Tanga na hali hiyo pia inaathiri juhudi za Serikali kupunguza gharama za kufanya biashara kumnufaisha mlaji wa mwisho.

Hivyo basi, EWURA inatoa **Agizo** kuwa mafuta yote yatakayotumika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara lazima yawe ni yale yaliyopitia Bandari ya Tanga na si vinginevyo.

Mtu yeyote atayekiuka Agizo hili atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa kifungu cha 238 cha sheria ya Petroli, Sura ya 392, na akipatikana na hatia adhabu yake ni faini si chini ya shilingi milioni 100 au kifungo cha miaka si chini ya 10 au vyote.

EWURA inafuatilia kwa karibu hali ya upatikanaji wa mafuta nchini ili kuhakikisha maslahi ya wadau wote wakiwemo watumiaji, makampuni ya mafuta na serikali yanalindwa.

Imetolewa na
Mkurugenzi Mkuu
EWURA